# TATHMINI YA PAMOJA YA MARANDA NA KISII

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari

## MTIHANI WA KIBAADA MWIGO 2021

**102/3** **KISWAHILI (FASIHI)** **Karatasi ya 3**

Januari 2021 – Saa: 2½

---

Jina : ............................................................ Nambari ya Usajili: ...............

Mkondo: ........... Sahihi ya mtahiniwa: ............. Tarehe: ......../01/2021.

---

*Maagizo*

a) *Jibu maswali **manne** pekee.*
b) *Swali la **kwanza** ni la **lazima**.*
c) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani: Riwaya, Hadithi Fupi, Tamthilia na Ushairi.*
d) *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
e) *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*
f) *Majibu yote sharti yaandikwe kwenye kijitabu cha majibu ulichopewa.*
g) *Karatasi hii ina kurasa **14** zilizopigwa chapa.*
h) *Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*
i) *Andika nambari kwa maswali uliyoyajibu kwenye jedwali ulilochorewa hapo chini.*

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

## SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

**1. Lazima**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*

Paukwa?
Pakawa.
Hapo zama, paliishi pandikizi la mtu mwenye miraba minne, lililokacha msuli na kuvudumka mwili. Lilikuwa na minywele kifuani kama simba na nguvu za ajabu. Aliitwa Mashoka. Siku moja kulizuka vita katika kijiji chao cha Vitakuu. Kina dada, mama na hata watoto wengi walitiwa vitanzi na mifugo kutwaliwa. Wanaume waliojitoa vitani walijaribu kadiri ya uwezo wao. Lakini Lo! Walilemewa na wapinzani hadi pale Mashoka alipoamua kujiiingiza vitani ili kuwanusuru wanajamii wenzake. Nguvu zake nyingi zilimpa uwezo wa kuvunja fupaja la mtu kwa kofi tu. Wapinzani walipomwona tu damu iliwaganda, wakabaki tutwe na wengine kujichafua papo hapo. Ghafla nyimbo za shangwe zilisikika zikimsifu Mashoka kwa kuwashinda wapinzani wake katika sherehe zilizodumu mwezi mzima.

*Tunaye Masho ... oooh! Mashoka, hamtamweza!*
*Tunaye Masho ... aaah! Mashoka, hamtatuweza!*
*Mashoka ... Mashoka ... Mashoka, milele!*

a) Tambua kipera cha utanzu wa ngano kinachohusishwa na kifungu hiki. Thibitisha jibu lako kwa mifano yoyote **mitatu**. (alama 4)

b) Fafanua majukumu **matano** ya kipera hiki katika jamii (alama 5)

c) Andika shughuli **moja** ya kijamii na **moja** ya kiuchumi ambazo huendelezwa katika jamii ya utungo huu. (alama 2)

d) Bainisha vipengele **vinne** vya kimtindo vilivyotumika kufanikisha uwasilishaji wa utungo huu. (alama 4)

e) Eleza faida za matumizi ya mbinu ya kushiriki katika utafiti wa fasihi simulizi. (alama 5)

## SEHEMU B: RIWAYA

Assumpta K. Matei : *Chozi la Heri*

*Jibu swali la 2 au 3*

**2.** " Ushaona? Hivi karibuni nchi inafikia *Vision 2030* hata kabla ya 2030 yenyewe!"

a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)

b) Kwa mifano **kumi na sita**, eleza mchango wa serikali katika kuimarisha maisha ya wananchi wake. (alama 16)

**3.** "Nyamaza wewe! Nyinyi ndio mlioturudisha nyuma miaka yote hii. Mnatuhadaa kwa vishahada mnavyotupa vyuoni, vishahada ambavyo ni laana kwetu..."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Eleza mbinu **tatu** za fasihi zilizotumika katika dondoo. (alama 3)

c) Eleza sifa **nne** za msemaji wa maneno haya. (alama 4)

d) Fafanua namna mbinu ya usimulizi ndani ya usimulizi ilivyotumika katika kuendeleza dhamira ya riwaya hii. (alama 9)

## SEHEMU C: TAMTHILIA

Pauline Kea: *Kigogo*

*Jibu swali la 4 au la 5*

**4.** "Na katika uchu huo huo amependa kukifikia kilele cha ufanisi kwa kukanyaga migongo ya wenziwe"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Huku ukitolea mifano **kumi na sita**, eleza jinsi siasa za unasaba zinavyoathiri maisha ya Wanasagamoyo. (alama 16)

**5.** "Wanaishia kuwa makabeji kwa kudungana sumu ya nyoka."

b) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

c) Fafanua kwa kutoa mifano, maana **nne** za kitamathali za istilahi "sumu ya nyoka." (alama 4)

d) Tathmini umuhimu **nne** wa msemaji wa maneno haya katika tamthilia. (alama 4)

e) "Asasi inayorejelewa inakumbwa na changamoto si haba." Fafanua kwa kutolea mifano **minane**. (alama 8)

## SEHEMU D: USHAIRI

*Jibu swali la 6 au la 7*

**6.** *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Ana kero duniani, mahuluki ale mwongo,
Haeleweki yakini, mamboye huwa fyongo,
Kukweleza natamani, nimeuanza mtungo,
Maisha ulimwenguni, ukweli ndiyo silaha.

Ataanza kwa anwani, kujisifu kwa madaha,
Huyo nakupa ilani, hana yoyote nasaha,
Anenayo ni matani, yatakutia jeraha,
Maisha ulimwenguni, ukweli ndiyo silaha.

Yamtokayo kinywani, ni machache ya furaha,
Ya ukweli kwa mhuni, ni uvundo na usaha,
Takutia mashakani, yake mengi ni mzaha,
Maisha ulimwenguni, ukweli ndiyo silaha.

Hutokea kisirani, mtalamu kudanganya,
Watu wengi humwamini, kiongozi kumfanya,
Siku chache huthamini, kisha hapo huwafinya,
Maisha ulimwenguni, ukweli ndiyo silaha.

Una sumu duniani, uongo wa kiongozi,
Huwapa matumaini, uahidi kibazazi,
Kimweka uongozini, anotenda si azizi,
Maisha ulimwenguni, ukweli ndiyo silaha

Hana bora na amani, mjinga mdanganyifu,
Ya ukweli akilini, ni mzaha kwa kipofu,
Mahuluki hamwamini, na wengi humkashifu,
Maisha ulimwenguni, ukweli ndiyo silaha.

Mwongo mmoja makini, waja kadha hupoteza,
Ni maradhi ja tauni, adinasi huwafiza,
Uongo si wa nuruni, huwatia watu giza,
Maisha ulimwenguni, ukweli ndiyo silaha.

Huja mengi maningani, heri uwe mnyamavu,
Yanotoka ubongoni, uyafanye adilivu,
Ya hekima uwekeni, sitamke mapotovu,
Maisha ulimwenguni, ukweli ndiyo silaha.

Mwongo hamchi Manani, humwogopa mtu mno,
Nimefika ukingoni, yangu hayo ndo maono,
Halifutiki jamani, liandikwalo kwa wino,
Maisha ulimwenguni, ukweli ndiyo silaha.

*(Ukweli – Nyamboga Daniel)*

a) Huku ukirejelea **hoja sita,** jadili wazo kwamba uwongo ni sumu hatari. (alama 6)

b) Eleza tamathali **mbili** za usemi zinazojitokeza katika shairi hili. (alama 4)

c) Tambua **nafsineni** katika shairi hili. (alama 2)

d) Eleza **toni** katika shairi hili. (alama 2)

e) Andika ubeti wa **nane** katika lugha nathari. (alama 4)

f) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo; (alama 2)

   i. Vipande
   ii. Ujumbe

7. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Beberu limepevuka,
Linatumia umwamba,
Na pia linajigamba,
Hivi sasa linatamba,
Kila pembe linafika.

Beberu lina jeuri,
Kwa walijualo,
Huenda litakalo,
Hufanya lipendalo,
Kwa dharau na kiburi.

Beberu bomani mwake,
Hakuna 'nosalimika,
Waliomo huwasaka,
Kila mmoja kufyeka,
Hutesa kwa pembe zake.

Beberu limejeruhi,
Wapo walo mahututi,
Na wengine ni hayati,
Yamewafika mauti,
Mbuzi dume 'mefurahi.

*(Beberu – K.W. Wamitila)*

a) Kwa **hoja sita,** jadili jazanda ya beberu na sifa zake katika shairi hili. (alama 6)
b) Tambua uhuru wa mshairi uliotumika katika shairi hili. (alama 2)
c) Changanua umbo la shairi hili. (alama 4)
d) Andika ubeti wa **mwisho** katika lugha ya nathari. (alama 4)
e) Eleza toni katika shairi hili. (alama 2)
f) Fafanua nafsineni katika shairi hili. (alama 2)

## SEHEMU E: HADITHI FUPI

Alifa Chokocho na Dumu Kayanda: *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*

**8.**

*"Ndoto ya Mashaka" (Ali Abdulla Ali)*

a) "Tuligandamana tukawa kitu kimoja – mie na waridi – mpaka pale dhoruba ilipotutenganisha."

i. Muktadha wa maneno haya. (alama 3)

ii. "Mzungumzaji wa maneno haya alipigwa na dhoruba mbalimbali maishani." Thibitisha. (alama 11)

*"Masharti ya Kisasa" (Alifa Chokocho)*

b) "Kwa hivyo, ukitaka kunioa lazima ufanye wajibu wa kisasa kwa mimi nitakayekuwa mkeo wa kisasa."

"Wahusika katika muktadha huu wana maoni tofauti kuhusu maisha." Thibitisha ukirejelea hoja **sita** katika hadithi *Masharti ya Kisasa.* (alama 6)

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................